KISWAHILI KARATASI 1

9

GREDI YA TISA - 2026

JINA:.....

SHULE:.....

NAMBARI YA USAJILI .....TAREHE: .....

Soma Kifungu Kifuatacho Kisha ujibu swali la 1-6.

Jamila alikuwa mwanamke mwenye bidii mithili ya mchwa. Kila siku ya Dominika Jamila aliamka asubuhi na mapema ili kufanya usafi wa nyumba. Hii ndiyo siku alisafisha kila sehemu ya nyumba, kutoa vumbi kwenye vifaa vyake, kutoa utando kwenye kuta na kunadhifisha chumba cha kuku wake. Bwana Musa, mume wake, alienda shambani kutafuta majani ya kulisha mifugo yao. Mtoto wao ambaye alikuwa na umri wa miaka mitano alikaa na bibi na kurejeshwa kwao wikendi.

Mara tu baada ya kukamilisha kula kiamshakinywa, Jamila alichukua ndoo ndogo mbili. Moja alitia maji yenye sabuni na nyingine maji safi yasiyo na sabuni. Alitia vitambaa viwili ndani yake. Alianza kwa kupangusa meza, viti na kabati. Baadaye alipangusa vioo vya madirisha na milango yote. Kila alipotumia maji yenye sabuni alirudia kwa maji yasiyo na sabuni kwa mara ya pili ili kuhakikisha sehemu hiyo imeng'aa.

Baada ya kumaliza kupangusa sehemu hizo, alichukua ndoo kubwa na taulo kuukuu. Alipiga deki sakafu yote huku akisafisha hadi mvunguni mwa makochi na vitanda. Alifanya hivyo ili kuzuia magonjwa yaletwayo na vumbi nyumbani kama vile mafua. Alipokamilisha kusafisha nyumba, alifululiza hadi kwenye chumba cha kuku na kuwafungulia kuku wake ili afagie. Alifagia na kunyunyizia dawa ya kuzuia funza kuwavamia kuku. Vilevile, alisafisha vyombo vyao vya chakula. Alisafisha vyombo hivi kila siku ili kuzuia magonjwa ya kuku.

Kwa kuhitimisha, Jamila alifagia nje ya nyumba na kuchoma taka za wiki nzima katika eneo lililotengewa kazi hiyo. Mume wake alipowasili alilengeta ua uliozunguka boma lao ili kuzuia mbu wasiwavamie. Baadaye Jamila aliandaa chakula na wote wakala wakifurahia mazingira safi.

1. Kila siku ya Dominika Jamila alifanya nini?
   A. Kulengeta na uliozunguka boma.
   B. Kufanya usafi nyumbani kwao.
   C. Kutafuta majani ya mifugo yao.
   D. Kwenda kwa bibi kumchukua mtoto wao.
2. Je, ni kazi gani kati ya hizi haikufanywa na Jamila siku ya Jumapili?
   A. Kufuta vumbi kwenye vifaa vya nyumba.
   B. Kupangusa madirisha na milango.
   C. Kukaa na bibi nyumbani.
   D. Kunadhifisha chumba cha kuku.
3. Je, unadhani ni nini kingetokea iwapo Jamila hangefanya usafi wa nyumbani?
   A. Wote wangepata magonjwa yanayotokana na uchafu.
   B. Kuku wake wangeongezeka kwa kula uchafu.
   C. Bwana Musa angefurahia mazingira hayo.
   D. Mtoto wao angefanya usafi wa nyumbani.
4. Ni jibu lipi linaloonyesha mfuatano ufaao wa matendo ambayo Jamila alifanya kila siku ya Dominika?
   A. Kufuta vumbi, kutafuta majani na kuandaa chakula.
   B. Kufagia chumba cha kuku, kufyeka nyasi, kupiga deki na kuandaa chakula.
   C. Kupiga deki, kupangusa vumbi, kuandaa chakula, na kufagia chumba cha kuku.
   D. Kufuta vumbi, kupiga deki, kufagia chumba cha kuku na kuandaa chakula.
5. Kauli **"Piga deki"** ni mbinu gani ya lugha?
   A. Nahau B. Methali
   C. Tashbihi D. Kitendawili
6. Uchafu wa vumbi husababisha ugonjwa wa:
   A. Malaria B. Malale
   C. Mafua D. Pumu